LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz Website www.humanrights.or.tz

# TAMKO KWA UMMA
# KUKOSEKANA KWA UMEME NCHINI NA UHUSIANO WAKE NA HAKI ZA BINADAMU

**Ndugu wanahabari,**
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimefuatilia na kufanya tathmini kuhusu hali ya kukatika kwa umeme na athari yake kwenye Haki za Binadamu na athari za kiuchumi.

Itakumbukwa kuwa tangu mwaka 2022 kumekuwa na changamoto ya kukatika katika kwa umeme bila taarifa kamili kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) hadi mwezi Septemba 2023 bila kuwepo kwa taarifa kamili kwa watumiAJI wa umeme nchini, hali iliyopelekea Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kufanya mabadiliko ya aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania Bwana Maharage Chande na kumteua Bwana Gissima Nyamo-Hanga.

Siku ya tarehe 26 mwezi wa 9, 2023 Rais Samia alitoa muda wa miezi (6) sita kwa shirika la umeme nchini TANESCO kushughulikia uboreshaji wa mitambo ya umeme ili kumaliza kabisa tatizo la kukatika kwa umeme, agizo hilo alilitoa jijini Dar es Salaam mara baada ya kumuapisha Mkurugenzi huyo mpya.

Siku chache mara baada ya kuapishwa kwa Mkurugenzi huyo, alitoa taarifa mbele ya waandishi wa habari alikieleza sababu kubwa ya katika kwa umeme kunatokana ni tatizo la upungufu wa uzalishaji kwa kiwango cha MEGAWATI 400 unaotokana na ukame uliosababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi uliyoathiri viwango vya maji katika mabwawa yanayotumiwa katika uzalishaji wa umeme.

Pia, ukarabati wa mitambo ya kuzalisha umeme ya UBUNGO Na. 1 na 2, mtambo wa gesi KINYEREZI EXTENSION 1 pamoja na visima vya kuzalisha gesi asilia. Mkurugenzi huyo alieleza matarajio ya Shirika la Umeme ni kutatua changamoto ya upungufu huo kwa wastani wa MEGAWATI 100 kila mwezi hivyo hadi kufikia mwezi Machi, 2024 tatizo

litakuwa limeisha kabisa. Hivyo sababu hizo zimepelekea kuwa na mgao wa umeme.

**Ndugu wanahabari,**
LHRC inatoa tamko hili kwa lengo la kuikumbusha Serikali kuwa, tatizo la kukatika kwa wa umeme linaathiri haki mbalimbali za kikatiba (Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977) ikiwemo, Ibara ya 22 na 23 inayobainisha haki ya kufanya kazi na kujipatia ujira, Ibara ya 14 haki ya uhai kwa kupata afya bora, na Ibara ya 18 haki ya kupokea na kutoa taarifa.

Hivyo, pamoja na jitihada za Serikali za kutatua changamoto za upungufu wa umeme nchini ni muhimu kuweka mikakati madhubuti ya kutafuta utatuzi wa kudumu wa upungufu wa umeme.

Tatizo la kukatika kwa umeme Tanzania limekuwa ni suala la linalojirudia mara kwa mara mbali ya kuwepo kwa utajiri wa vyanzo mbalimbali vya uzalishaji ikiwemo gesi asilia inayozalishwa Mtwara na Lindi katika maeneo mbalimbali ikiwemo Songo Songo, Mnazibay Msimbati na Madima.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Bwana Mussa Mohamed Makame alisema viwango vya uzalishaji wa gesi katika visima vitano (5) vya Mnazibay Msimbati umeongezeka ambapo zaidi ya asilimia 85 inayozalishwa katika vitalu hivyo huenda katika uzalishaji wa umeme nchini na kufanya mchango wa gesi asilia kuzalisha nishati hiyo kwenye grid ya taifa kwa **asilimia 70,** taarifa aliyoitoa siku ya tarehe 28 Septemba , 2023 mkoani Mtwara.

**Ndugu wanahabari,**
Ni wazi kuwa Tanzania ina utajiri mkubwa wa vyanzo mbalimbali vya kuzalisha umeme, kuendelea kwa tatizo la mgao wa umeme kwa kujirudia rudia umesababisha usumbufu mkubwa sana kwa wananchi, hususan katika shughuli za kila siku za maisha kama vile uzalishaji, biashara, huduma za afya na elimu.

**Ndugu wanahabari**
Mbali na changamoto zote hizi wanazopitia watanzania hakuna mtu aliyewajibika kwa ukosefu wa umeme. Wakati Serikali ilishatoa ahadi ya kuhakikisha umeme unapatika Machi 2024. Bunge limeshindwa kusimamia kuhakikisha ahadi hii ya Serikali inatekelezwa kinyume chake tumeona hivi karibuni Bunge likiongeza muda Serikali hadi Juni

2024. Serikali imekuwa inatoa ahadi hewa mara nyingi toka kipindi cha mradi wa gesi kuwa tatizo la umeme Tanzania limeisha lakini mbali na hizi ahadi kuwa hewa hakuna aliyewajibika hadi leo.

Jambo hili limeendelea kuleta hali ya sintofahamu ikilinganishwa na utajiri wa rasilimali na maliasili za vyanzo vya kuzalisha nishati ya umeme. Kukatika wa umeme kuna athari kubwa kwa jamii na uchumi wa nchi. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na:

**Usumbufu katika Maisha ya Kila Siku**
Usumbufu katika Shughuli za Kila Siku: Kukatika kwa umeme husababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi katika shughuli zao za kila siku kama vile kupikia chakula, kuendesha biashara ndogo, na kuendeleza shughuli za kielimu. Wananchi wanaweza kulazimika kurekebisha ratiba zao na kutumia muda mwingi kutafuta njia mbadala za kupata umeme ili kukidhi mahitaji yao yanayotegemea nishati hiyo.

**Athari kwa Huduma za Afya**
Athari kwa Huduma za Afya: Sekta ya afya hutegemea matumizi ya umeme ili kutoa huduma kwa wagonjwa katika vituo vya afya na hospitalini. Kukosekana kwa umeme kunaweza kusababisha kusitishwa au kupunguzwa kwa huduma za matibabu, hali ambayo inahatarisha haki ya uhai kwa wagonjwa.

Hivyo, athari ya kukatika kwa umeme kunahatarisha haki ya uhai kwa kuwa kwa kiwango kikubwa huduma za afya za dharura hutegemea matumizi ya nishati ya umeme, hivyo kukosekana na kwa nishati hiyo ni tisho dhidi ya haki ya kuishi kama ilivyobainishwa katika **Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Mfano kuna Watoto wanaizaliwa kabla ya muda wanaitakiwa kukaa katika uangalizi maalum ambapo mitambo yake inatumia umeme.**

**Athari kwa Biashara na Viwanda**
Athari kwa Biashara na Viwanda: Wananchi wanaweza kupata hasara katika biashara zao na uzalishaji katika viwanda kutokana na kukatika kwa umeme. Hii inaweza kusababisha kupungua kwa mapato ya kaya, kupoteza ajira, na hata kufungwa kwa biashara na viwanda vidogo. Hii ina athari kubwa kwa uchumi wa nchi na maisha ya watu.. Hivyo, kukosekana kwa nishati ya umeme kunathiri haki ya mtu kufanya kazi kama inavyobainishwa katika **Ibara ya 22 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.**

**Kuongezeka kwa gharama za Maisha**
Kuongezeka kwa Gharama za Maisha: Wananchi wanaojitahidi kupata umeme mbadala kama vile jenereta au solar wanaweza kukabiliwa na gharama kubwa za kununua na kuendesha vifaa hivyo. Hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za maisha na kupungua kwa ufanisi wa kiuchumi kwa wananchi.

Kwa ujumla, kukosekana kwa umeme kunaweza kusababisha athari kubwa kiuchumi na kijamii kwa jamii na uchumi wa nchi, na inahitaji suluhisho la haraka na la kudumu ili kuboresha upatikanaji wa nishati ya umeme.

**Ndugu wanahabari,**
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kinamapendekezo yafuatayo;

1. Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana ndani ya muda mfupi. Hili linawezekana kwani tumeshuhudia miaka zaidi ya sita hapa karibuni nchi ilikuwa na umeme wa uhakika.

2. Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kupanga ratiba ya matengenezo ya mitambo ya kuzalisha umeme kwa kuzingatia sayansi ya mabadiliko ya tabia ya nchi, mathalani siku ya tarehe **23 mwezi Novemba, 2022 TANESCO** ilitoa taarifa kwa umma juu ya hali ya upungufu wa umeme na mpango wa kukabiliana nao, katika taarifa hiyo TANESCO lisema inapitia kipindi kigumu cha upungufu wa umeme kwa sababu ya ukame na matengenezo ya mitambo.

3. Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutoa taarifa zisizokuwa na mkanganyiko kwa umma.

- Mathalani, mnamo tarehe **12 mwezi Septemba 2023** aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO Bwana Maharage Chande alisema kuwa kutokana na upungufu wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme nchini, ikiwa mvua zitachelewa kutakuwa na uhaba wa umeme.

- Hata hivyo katika kipindi cha mwezi Oktoba na Novemba mvua kubwa zilinyesha katika mbalimbali nchini, ambapo tarehe **24 mwezi Novemba 2023** Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika Mhandisi Gissima

Nyamo-Hangahilo alisema kuwa mtiririko wa maji ya mvua hizo haulekei kwenye vyanzo vya uzalishaji wa umeme vya Mtera, Kidatu na Kihansi.

4. Serikali kuongeza uwekezaji katika vyanzo vya uzalishaji wa nishati ya umeme isiathirika kirahisi na mabadiliko ya hali ya hewa. Pendekezo hili linalenga kuongeza upatikanaji endelevu wa nishati ya umeme kwa changamoto ya mabadiliko ya tabia ya nchi huathiri kwa kiasi kikubwa upungufu wa uzalishaji wa umeme.

**Imetolewa leo tarehe 19 Februari, 2024 na;**
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)**

**Dkt. Anna Henga**
**Mkurugenzi Mtendaji**